# JIFUNZE Kusali



**Tafadhali wakumbukeni wafuatao kwa kisomo cha Suratu Al-Fatihah**

Marehemu Gulamhusain Mawji
Marehemu Bi-Zera Bai Gulamhusain Mawji
Marehemu Naheed Masumali Shamji
Marehemu Ali Sajid Walji
Marehemu Abdul Lalji
Marehemu Sayed Abbas Al Musawy (Znz)
Marehemu Hussein Abbas
Marehemu Ally Hussein Abbas
Marehemu Shakur Ramin

Marehemu wote wa ufungu wa:
Mawji
Shamji
Rattansi
Alimuhammad
Shakur
Dewji
Kermali
Dhanani
Bharwani
Nakhuda
Rajani
Chandoo
Walji
Jaffer
Khimani
Pardhan
Jafferali Merali

ASK
www.ask.or.tz
Discuss | Debate | Share | Learn

بسم الله الرحمن الرحيم

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu,*
*Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

# Sala

"E-nyi wanadamu! Mwabuduni Mola wenu aliekuumbeni ninyi na aliewaumba waliekutangulieni, ili mfikilie uchaji"
**(Suratu Al-Baqarah, 2:21)**

Sala inaainisha sifa njema kumi:
Ni nguzo ya imani, inahaibisha uso, inanawirisha moyo, inafarajisha mwili, ni sahibu kaburini, inarehemesha, ni mwangaza wa mbingu, inaipa nguvu uzani (hukumu), inamfurahisha Mwenyezi Mungu, ni tuzo la peponi na ni kiziwizi cha motoni. Mwenye kupuza sala, amejiangamiza.
**(Mtukufu mtume – SAWW)**

Ipe sala umuhimu na itekeleze kwa wakati hasa upasao. Ikabilishe kwa uwezo wako wote, kwa nia ya kumkurubia Mwenyezi Mungu. Ni faradhi kwa mwamini kusimamisha sala kwa wakati aliopangiwa.
**(Imam Ali Ibnu Abi Talib – AS)**

# Adhana

## *(Wito wa Sala)*

Wakati wa sala unapoingia, sauti ya adhana husikika kutoka katika kila msikiti. Ni utaratibu uliotiliwa nguvu ufanyike ili waumini wajiandae kwa sala. Yafuatayo ni taratibu zake:

**Ita mara 4:**

اللّٰهُ أكبَر

ALLĀH-U AKBAR

*Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

**Ita mara 2:**

أَشْهَدُ أَنْ لا إلهَ إلّاللّٰهُ

ASHHAD-U AN LĀ ILĀH-A ILLĀLLĀH

*Nashuhudia ya kuwa hakuna mungu (mwengine) ila Mwenyezi Mungu*

**Ita mara 2:**

أَشهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ الله

ASHHAD-U ANNA MUḤAMMAD-AN RASŪLULLĀH

*Nashuhudia ya kuwa Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu*

**Ita mara 2:**

أَشْهَدُ أَنَّ عَليّاً وَلِيُّ اللّٰهُ

ASHHAD-U ANNA ALĪ-YYAN WALĪ-YYULLĀH

*Nashuhudia ya kuwa Ali ni kaimu wa Mwenyezi Mungu*

**Ita mara 2:**

**حَيَّ على الصَّلاة**

HAYYA ‘ALĀS-SALĀH

*Jihimize kwa sala*

**Ita mara 2:**

**حَيَّ على الفَلاح**

HAYYA ’ALĀ L-FALĀH

*Jihimize kunako kiokozi*

**Ita mara 2:**

**حَيَّ على خَيْرِ العَمَل**

HAYYA ‘ALĀ KHAYRIL ’AMAL

*Jihimize katika kitendo kilicho bora*

**Ita mara 2:**

**اللّٰهُ أكبَر**

ALLĀH-U AKBAR

*Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

**Ita mara 2:**

**لا إلهَ إلّاالله**

LA ILĀH-A ILLĀLLĀH

*Hakuna mungu (mwengine) ila Mwenyezi Mungu*

# Iqama

## *(Mwinuko kwa Sala)*

Baada ya adhana, kinachofuatia ni sala. Mwamini anatakiwa kusimama imara, tayari na mwangalifu kwa sala, aelekee qibla. Wito wa mwinuko wa sala unaitwa “Iqama” kama ifuatayo:

**Ita mara 2:**

**اللّٰهُ أكبَر**

ALLĀH-U AKBAR

*Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

**Ita mara 2:**

**أَشْهَدُ أَنْ لا إلهَ إلّاللّٰهُ**

ASHHAD-U AN LĀ ILĀH-A ILLĀLLĀH

*Nashuhudia ya kuwa hakuna mungu (mwengine) ila Mwenyezi Mungu*

**Ita mara 2:**

**أَشهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ الله**

ASHHAD-U ANNA MUḤAMMAD-AN RASŪLULLĀH

*Nashuhudia ya kuwa Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu*

**Ita mara 2:**

**أَشْهَدُ أَنَّ عَليّاً وَلِيُّ اللّٰهُ**

ASHHAD-U ANNA ALĪ-YYAN WALĪ-YYULLĀH

*Nashuhudia ya kuwa Ali ni kaimu wa Mwenyezi Mungu*

**Ita mara 2:**

**حَيَّ على الصَّلاة**

HAYYA ‘ALĀS-ṢALĀH

*Jihimize kwa sala*

**Ita mara 2:**

**حَيَّ على الفَلاح**

HAYYA ’ALĀ L-FALĀH

*Jihimize kunako kiokozi*

**Ita mara 2:**

**حَيَّ على خَيْرِ العَمَل**

HAYYA ‘ALĀ KHAYRIL ’AMAL

*Jihimize katika kitendo kilicho bora*

**Ita mara 2:**

**قَدْ قامَت الصّلاة**

QAD QĀMAT-IṢ-ṢALĀH

*Jiinushe kwa sala*

**Ita mara 2:**

**اللّٰهُ أكبَر**

ALLĀH-U AKBAR

*Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

**Ita mara 1:**

**لا إلهَ إلّااللّٰهُ**

LA ILĀH-A ILLĀLLĀH

*Hakuna mungu (mwengine) ila Mwenyezi Mungu*

# Sala

Nyakati za sala na rakaa zake:

1. Sala ya alfajiri ina rakaa 2
2. Sala ya adhuhuri ina rakaa 4
3. Sala ya alasiri ina rakaa 4
4. Sala ya magharibi ina rakaa 3
5. Sala ya Isha ina rakaa 4

# Nia

Tamko la nia iwe kwa mdomo au kwa moyo unaposimama kwa maandalizi ya sala, kama ifuatavyo:

(1)
Nanuia sala ya faradhi ya alfajiri yenye rakaa 2 kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke Yake

(2)
Nanuia sala ya faradhi ya adhuhuri yenye rakaa 4 kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke Yake

(3)
Nanuia sala ya faradhi ya alasiri yenye rakaa 4 kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke Yake

(4)
Nanuia sala ya faradhi ya magharibi yenye rakaa 3 kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke Yake


(5)

Nanuia sala ya faradhi ya Isha yenye rakaa 4 kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke Yake

**Rakaa ya Kwanza**

## Qiyam

*(Usimeme)*



Rakaa ya kwanza inaanza kwa kusimama wima inaitwa “qiyam” na baada ya kutia nia ya sala kisha tamka takbira tukufu iitwayo “Takbiratu Al-Ihram”

# Takbiratu Al Ihram

## (Takbira Tukufu)

Takbira tukufu inafanyika kama ifuatavyo:
Inua mikono yako miwili, vitanga vyake vifikie usawa wa masikio katika hali ya kusimama wima kisha utamke mara moja

**اللّٰهُ أكبَرَ**

ALLĀH-U AKBAR

*Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

**Kiendeleo cha Qiyam**

Baada ya takbira tukufu, teremsha mikono na uinyoshe kunako mapaja kisha uanze kusoma suratu Al-Fatihah mara moja

**بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ**

BISMILAHIR-RAHMAANIR-RAHEEM

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu*

**ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَـٰلَمِينَ**

ALHAMDU LILLAAHI RABBIL ‘AALAMEEN

*Sifa njema zote ni Zake, Mola wa ulimwengu*

**ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ**

AR-RAHMAANIR-RAHEEM

*Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu*

مَـٰلِكِ يَوْمِ ٱلدِّينِ
MAALIKI YAWMID-DEEN
*Ni Mfalme wa siku ya hukumu*

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ
IYYAAKA NA’BUDU WA IYYAAKA NASTA’EEN
*Wewe pekee wa kuabudiwa na Wewe pekee wa kukidhi haja*

ٱهْدِنَا ٱلصِّرَٰطَ ٱلْمُسْتَقِيمَ
IHDINAS-SIRAATAL-MUSTAQEEM
*Tuongoze katika njia iliyonyoka,*

صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ ٱلْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا ٱلضَّآلِّينَ
SIRAATAL-LADHEENA AN’AMTA ‘ALAIHIM
GHAYRIL-MAGHDHOOBI ‘ALAIHIM
WA LAD-DHAAALLEEN
*Njia ya hao uliewaenemesha, si njia ya wale ulieghadhabika nao kwa upotovu*

Baada ya kisomo cha Fatihah tu, utaendelea kwa kusoma suratu Al-Ikhlas mara moja

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ
BISMILAHIR-RAHMAANIR-RAHEEM
*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu*

قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ

QUL HUWAL LAAHU AHAD

*Tamka, Mwenyezi Mungu ni Pekee*

ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ

ALLAH HUS-SAMAD

*Mwenyezi Mungu ni huru wa hitaji*

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ

LAM YALID WA LAM YOOLAD

*Hakuzaa wala hakuzaliwa*

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَد

WA LAM YAKUL-LAHOO KUFUWAN AHAD

*Na hana mlinganifu Wake*

Kisha inua mikono yako, vitanga vyake vifikie usawa wa masikio kwa kusoma “Takbira (Mwenyezi Mungu ni Adhimu)” teremsha mikono kwa kujiandaa kuinama (rukuu)

# Rukuu

## (Mwinamo)



Soma mara moja:

سُبْحانَ رَبِّىَ الْعَظيمِ وَ بِحَمْدِه

SUBHAN-A RABBI-AL-'AZIM-I WA BI-HAMDIH

*Sifa njema zote ni za Mola wangu Adhimu na ni Mtukufu*

اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَ آلِ مُحَمَّد

ALLĀHUMMA ṢALLI ‘ALĀ MUḤAMMADIN WA ĀALI MUḤAMMAD

*E-we Mola! zifikishe baraka Zako kwa Muhammad na aqraba za Muhammad (salawati)*

Baada ya kisomo cha rukuu, inuka wima na kusoma mara moja


سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ

SAMI'ALLAHU LIMAN HAMIDAH

*Mwenyezi Mungu amesikia wito wa mwenye kumtukuza*

*Hapo tena utasoma “Takbira (mwenyezi Mungu ni Adhimu - kwa utaratibu kama ulivyoelezwa huko nyuma) kwa kujiandaa kwenda fudifudi (Sijida)*

## Sijida



Soma mara moja:

سُبْحانَ رَبِّىَ الْاَعلى وَ بِحَمْدِهِ

SUBHAN-A RABBI-AL-A'LA-WA BI-HAMDIH

*Sifa njema zote ni za Mola wangu Alietukuka na ni Mtukufu*

ٱللَّهُمَّ صَلِّ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَ آلِ مُحَمَّدٍ

ALLĀHUMMA ṢALLI ʻALĀ MUḤAMMADIN WA ĀALI MUḤAMMAD

*E-we Mola! zifikishe baraka Zako kwa Muhammad na aqraba za Muhammad (salawati)*

Kisha inua kichwa chako kwa kukaa kitako na kusoma "Takbira" mara moja, baada ya hapo soma mara moja

أَسْتَغْفِرُ ٱللَّهَ رَبِّي وَأَتُوبُ إِلَيْهِ

ASTAĠFIRU-LLĀHA RABBĪ WA-ATŪBU ILAYH

*Naomba msamaha Kwake Mwenyezi Mungu, Mola wangu na kujirudi mbele Yake*

Kisha soma "Takbira" mara moja kwa kujiandaa kwenda katika sijida ya pili. Kisomo cha sijida ya pili kitakuwa kama kisomo cha sijida ya kwanza

Baada ya kumaliza sijida ya pili, inua kichwa chako kwa kukaa kitako na usome "Takbira"

Baada ya "Takbira" inuka wima huku ukisoma

بحول الله وقوته أقوم وأقعد

BI-HAW-LILLAHI WA QUWWATIHI AQUMU WA AQU'D

*Mwinuko na ukao wangu umefadhilishwa kwa uwezo na nguvu za Mwenyezi Mungu*

## Rakaa ya Pili

Rakaa ya pili inaanza kwa kusimama wima (qiyam), punde tu baada kusimama, soma suratu Al-Fatihah kama ulivyosoma katika rakaa ya kwanza. Baada ya kumaliza suratu Al-Fatihah, endelea na qiyam kwa kusoma suratu Al-Ikhlas, umalizapo tu, una hiyari ya kusoma “Kithibitisho” kifuatacho:

**كذلك الله ربى**

KADHAALIKA-LLAHU RABBI

*Huyo ni Mwenyezi Mungu, Mola wangu*

*Angalia: Kisomo cha “Uthibitisho” kinasomwa baada ya suratu Al-Ikhlas tu, si vinginevyo (mara moja, mara mbili ama mara tatu)*

Kisha unasoma “Takbira” mara moja

# Qunuti

*(Dua)*



Kabla ya kwenda rukuu katika rakaa ya pili, inua mikono yako yote miwili na kuyaunganisha, viganja vyake vielekeze mbinguni, kisha soma dua ifuatayo:

ٱللَّٰهُمَّ صَلِّ عَلَىٰ مُحَمَّد وْ آل مُحَمَّد

ALLĀHUMMA ṢALLI ‘ALĀ MUḤAMMADIN WA ĀALI MUḤAMMAD

*E-we Mola! zifikishe baraka Zako kwa Muhammad na aqraba za Muhammad (salawati)*

رَبَّنا آتِنا فِى الدُّنْيا حَسَنَةً وَ فِى الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَ قِنا عَذابَ النَّار

RABBANA ATINA FI D-DUNYA HASANAT-AN WA FIL-AKHIRATI HASANATAN WA QINA 'ADHAB-AN-NAR

*E-we Mola! Tukidhie mema ya hapa duniani na mema ya ahera na tuokoe na adhabu ya moto*

اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَىٰ مُحَمَّد وَ آل مُحَمَّد

ALLĀHUMMA ṢALLI ‘ALĀ MUḤAMMADIN WA ĀALI MUḤAMMAD

*E-we Mola! zifikishe baraka Zako kwa Muhammad na aqraba za Muhammad (salawati)*

Angalia: Dua ilioandikwa juu ni moja kati ya dua zinazotumika mara kwa mara, lakini ni hiyari ya mtu kusoma dua nyinginezo

Baada ya qunuti, soma “Takbira” kwa kujiandaa kwa rukuu na sijida kama ilivyoelezwa huko nyuma

# Hali ya Ukao



Hali ya ukao baina ya sijida mbili na wakati wa kusoma tashahudi na salamu

## Tashahudi

*(Shahada)*

Baada ya kumaliza sijida ya pili na kusoma “Takbira” tulia kwa kukaa kitako na kusoma yafuatayo:

ٱلْحَمْدُ للهِ

اَشْهَدُ اَنْ لااِلهَ اِلاَّ اللّهُ وَحْدَهُ لاشَرِيكَ لَهُ، وَاَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَداً

عَبْدُهُ وَ رَسُولُه، اَللّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّد وَ آلِ مُحَمَّد

AL-ḤAMDU LILLĀH. ASHHADU AN-LA ILAHA ILLAL-LAH, WAHDAHU LA SHAREEK-ALLAH, WA ASHHADU ANNA MUHAMMADAN ABDUHU WA RASULUH. ALLAHUMMA SALLI 'ALA MUHAMMADIN WA AALI MUHAMMAD

*Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Nashuhudia ya kuwa hakuna mungu (mwengine) ila Mwenyezi Mungu. Nashuhudia ya kuwa Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu. E-we Mola! zifikishe baraka Zako kwa Muhammad na aqraba za Muhammad*

## Salamu

*(Maamkizi)*

Ukiendelea na ukao huo huo, unganisha na kusoma kifuatacho:

اَلسَّلامُ عَلَيْكَ اَيُّهَا النَّبيُّ وَ رَحْمَةُ اللّهِ وَ بَرَكاتُهُ، اَلسَّلامُ عَلَيْنا وَ عَلى عِبادِ اللّهِ الصّالِحينَ، اَلسَّلامُ عَلَيكُمْ وَ رَحْمَةُ اللّهِ وَ بَرَكاتُهٌ

AS-SALAMU 'ALAYK-A AYYUHAN-NABIYYU WA RAHMATU-LLAH-I WA BARAKATUH, AS-SALAMU 'ALAYNA WA 'ALA 'IBADIL-LLAHI SSALIHEEN, AS-SALAMU 'ALAYKUM WA RAHMAT-UL-ALLAH-I WA BARAKATUH

*Amani ya Mwenyezi Mungu ishuke juu yako, e-we mtume! pamoja na rehema na baraka Zake. Amani ya Mwenyezi Mungu ishuke juu yetu na juu ya waja wema. Amani ya Mwenyezi Mungu ishuke juu yenu nyote pamoja na rehema na baraka Zake*

**Mwishowe**

Soma "Takbira" mara tatu za kuhitimisha sala

Huu ni mwisho wa sala ya alfajiri yenye rakaa mbili

## Rakaa ya Tatu

Sala zenye rakaa zilizozidi mbili taratibu zake zitakuwa kama ifuatavyo:

Baada ya "Tashahudi" inuka wima "Qiyam" kama ilivyoelezwa kabla na usome "Tahlili" iitwayo "Tasbihatu Arba'a" mara tatu badala ya sura za Qur'ani

# Tasbihatu Arba'a

*(Tahlili Nne)*

سُبْحانَ اللّهِ وَ الْحَمْدُ لِلّهِ وَ لاإلهَ اِلّا اللّهُ وَ اللّهُ أكْبَر

SUBHAN ALLAHI WAL-HAMD-U LILLAHI WA LA ILAH-A ILLA ALLAHU WA-LLAH-U AKBAR

*Utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, na hakuna mungu (mwengine) ila Mwenyezi Mungu peke Yake, na Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

Kwa sala ya magharibi, baada ya kisomo hiki, nenda katika rukuu, sijida mbili, tashahudi na kumalizia kwa salamu na takbira tatu

**Rakaa ya Nne**

Sala zenye rakaa nne ni za adhuhuri, alasiri na isha. Baada ya sijida ya pili ya rakaa ya tatu inuka wima "Qiyam" kwa kusoma "Tasbihatu Arba'a" mara tatu vile vile, baada ya hapo malizia sala kwa rukuu, sijida mbili, tashahudi, salamu na takbira tatu.

Imependekezwa kuvuta uradi wa Bibi Fatimatu Zahra (SA) baada ya kila sala kama ifuatavyo:

# Tasbihatu Fatimata Zahraa (SA)

## Soma mara 34:

اللّٰهُ أكبَر

ALLĀH-U AKBAR

*Mwenyezi Mungu ni Adhimu*

## Soma mara 33:

ٱلْحَمْدُ للهِّٰ

AL-ḤA̋ḾDU LILLĀH

*Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu*

## Soma mara 33:

سُبْحَانَ ٱللهِّٰ

SUBH̋AAN ALLAAH

*Mwenyezi Mungu ni Mtukufu*

# Dua

**بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ**
**رَضِيتُ بِالله رَبّاً، وَبِمُحَمَّد صلىاللهعليهوآله نَبِيّاً، وَبِالاِسْلامِ**
**دِيناً، وَبِالقُرْآنِ كِتاباً وَبِالكَعْبَةِ قِبْلَةً، وَبِعَلِيٍّ وَلِيّاً وإِماماً،**
**وَبِالحَسَنِ وَالحُسَيْنِ وَعَلِيِّ ابْنِ الحُسَيْنِ وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ**
**وَجَعْفَرِ بْنِ مُحَمَّدٍ وَمُوسى بْنِ جَعْفَرٍ، وَعَلِيِّ بْنِ مُوسى وَمُحَمَّدِ**
**بْنِ عَلِيٍّ، وَعَلِيِّ بْنِ مُحَمَّدٍ وَالحَسَنِ بْنِ عَلِيٍّ وَالحُجَّةِ بْنِ الحَسَنِ**
**صَلَواتُ الله عَلَيْهِمْ أَئِمَّةً. اللّهُمَّ إِنِّي رَضِيتُ بِهِمْ أَئِمَّةً فَارْضِنِي**
**لَهُمْ إِنَّكَ عَلى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ**

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu*

*Nimejitosheleza kwa fahari ya kuwa Mwenyezi Mungu ni Mola wangu, Muhammad (SAWW) ni mtume wangu, dini ya kiislamu ni dini yangu, Qur'an ni kitabu kinachoniongoza, Ka'ba ni kielekeo changu cha ibada, Ali ni kaimu na imamu akifuatwa na Hasan, Husain, Ali mtoto wa Husain, Muhammad mtoto wa Ali, Jafar mtoto wa Muhammad, Musa mtoto wa Jafar, Ali mtoto wa Musa, Muhammad mtoto wa Ali, Ali mtoto wa Muhammad, Hasan mtoto wa Ali na Mahdi mtoto wa Hasan (Baraka za Mwenyezi Mungu ziwashukie) ni maimamu. E-we Mwenyezi Mungu! Nimejitosheleza kwa fahari ya kuwa wote hao ni maimamu wangu, nijaalie niwe msingi wa furaha kwao. Hakika Wewe ni Mweza wa kila jambo.*

# Notes

# Notes

Ask
www.ask.or.tz
Discuss | Debate | Share | Learn

www.ask.tz asktz ask.or.tz